

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Telegram “AFYA”, DODOMA
Nambari ya Simu: +255 026 – 2323267
E- Mail Na. ps@afya.go.tz



Mji wa Serikali Mtumba,
Barabara ya Afya,
S.L. P 743,
40478 DODOMA.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

TAARIFA YA MWENENDO WA UGONJWA WA CORONA (COVID-19) NCHINI

Dar es Salaam, Jumanne Aprili 07, 2020

WAGONJWA WAWILI WAPONA, ARUSHA HAKUNA MGONJWA

Wagonjwa wawili wa virusi vya Corona (COVID-19) waliokuwa wakipata matibabu katika vituo vya kutolea huduma ya afya katika majiji ya Dar es Salaam na Arusha wamepona na kufanya jumla ya wagonjwa waliopona kufikia watano huku mkoa wa Arusha kutokuwa na mgonjwa.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mheshimiwa Ummu Mwalimu amewashauri wananchi hao walioruhusiwa kurudi majumbani mwao kujikinga na maambukizi mengine ya virusi vya corona huku akiwataka wananchi kutowanyanyapaa watu waliopona maambukizi ya virusi hivyo.

Amesema kwa sasa mikoa ya Arusha na Kagera haina mtu mwenye maambukizi ya virusi vya corona na wagonjwa 18 wanaendelea vyema kupata matibabu kwenye vituo maalum vya kutolea tiba nchini isipokuwa mgonjwa mmoja hayupo katika hali ya kuridhisha.

Aidha, Wananchi wametahadharishwa kujiepusha kupata maambukizi ya virusi vya corona (COVID -19) kwa kuwa kuna taarifa za kuwepo kwa maambukizi ya ndani ya virusi hivyo.

Amesema Serikali itahakikisha inazuia maambukizi mapya ya virusi vya corona kutoka nje ya nchi kwa kuwaweka karantini wasafiri wote wanaoingia nchini ili kuhakikisha wenye maambukizi ya virusi hivyo hawaendi kusambaza kwa jamii.

Waziri Ummu Mwalimu ameyasema hayo leo jijini Dar es Salaam wakati akikabidhi matanki 350 kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa ajili ya kuweka katika maeneo yenye mikusanyiko ya watu ili kunawa mikono kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona. Matanki hayo ni kati ya matanki 1,000 yaliyotolewa na umoja wa wafanyabiashara wazalendo wa mkoa wa Dar es Salaam kwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Kasisim Majaliwa hivi karibuni.

Ameagiza mikoa yote nchini kuchukua hatua za kuwaweka karantini kwa siku 14 wasafiri wote wanaoingia nchini kutoka nje ya nchi huku akiahidi kushughulikia changamoto zilizojitokeza kwenye hosteli za wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam maarufu kama “hostel za Magufuli” zinazotumika kama karantini kwa mkoa wa Dar es Salaam.

Akipokea Matanki hayo kwa niaba ya mikoa yote nchini itakayopata matanki 26 kila mkoa, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mheshimiwa Paul Makonda amesema wasafiri wote wanaotoka nje ya nchi watawekwa hosteli ya Magufuli kwa siku 14 kwa lengo la kudhibiti mlipuko wa virusi vya corona jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Makonda amesema wasafiri wanaoishi katika hosteli hizo wanaruhusiwa kuingia na vitu vyao vikiwemo mashuka, mito na vinginevyo ambavyo havitaruhusiwa kutoka nje ya eneo hilo kwani vitateketezwa kulingana na miongozo na taratibu za afya.

Tanzania imetibitisha kuwa na jumla ya kesi Ishirini na Nne (24) za wananchi walioambukizwa virusi vya COVID-19 ambapo kesi 17 zimethibitishwa Tanzania Bara huku visiwani Zanzibar kuthibitisha kuwa na kesi 7 . Kifo kimoja kimethibitishwa kutokea Dar es Salaam.

Imetolewa na;



Gerard Chami

**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO**